Mauzo >>>Serikali imeuza tani milioni 1.3 za makaa ya mawe zenye thamani ya zaidi ya dola milioni 144.9

TASAF yafanikisha ujenzi kituo cha mabasi Lundusi

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amezindua rasmi kituo cha mabasi cha Lundusi kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mradi uliotekelezwa kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF) awamu ya pili kwa kushirikiana na wananchi wa Kijiji cha Lundusi.

Akizungumza katika uzinduzi huo juzi, Kanali Ahmed alisema kuwa TASAF ni nyenzo muhimu ya kupambana dhidi ya umaskini kwa kuwa unawawezesha wananchi kutumia fursa za kuinua hali zao za kiuchumi.

Alisema kuwa kuwa awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango wa TASAF, umejikita katika masuala ya kuwezesha kaya kutumia fursa za kukuza uchumi na kuongeza kipato katika kaya za walengwa.

Pia, mradi huo umelenga kuboresha upatikanaji huduma za afya, elimu, maji safi na salama pamoja na miundombinu ya kukuza uchumi katika ngazi ya jamii.

Alisema kuwa ujenzi wa kituo cha mabasi pamoja na maduka ya biashara katika eneo hilo ni hatua muhimu ya kuimarisha uchumi wa kaya na jamii kwa ujumla, hivyo alitoa wito kwa viongozi na wananchi kulitunza miundombinu hiyo iendelee kutoa manufaa kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray, alisema kuwa TASAF iliboa sh. milioni 686.3 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha mabasi baada ya kupokea maombi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa mpango wa kunusuru kaya maskini mwaka 2001, umekuwa ikitoa ruzuku kwa halmashauri nchini kwa lengo la kuwawezesha walengwa ambapo hadi kufikia sasa jumla ya Sh. trilioni 1.17 zimetolewa kuwafikia walengwa.

Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Mary Makondo, alisema kuwa mkoa huo utaendelea kushirikiana kwa karibu na TASAF ili kuhakikisha miradi iliyobaki inakamilika kwa wakati.



Maofisa ugani waagizwa kuwatembelea